**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari MKOLANI**
**S.L.P.11638 –**
**MWANZA**

**Tarehe . 18/04/2024**

**Namba za simu**

**Mkuu wa Shule 0784 932097**

**Makamu Mkuu wa Shule 0719 223241**

**Matron/ 0786 897462**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah:**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE Y SEKONDARI MKOLANI HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA MKOA WA MWANZ MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katik Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ………….


Shule ya Sekondari MKOLANI ipo umbali wa Kilometa 08 Kutoka katikati ya jiji la Mwanz Kwa wale wanaokuja kwa magari (Mabasi) kutoka Mikoani,shule ipo umbali wa takriba kilometa 1 kutoka kituo Kikuu cha mabasi Nyegezi.(Nyegezi Bus Terminal)

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2024 Mwisho wa kuripoti shuleni ni 14/07/2024

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni Sketi 2 za damu ya mzee kwa Wasichana(kitambaa cha suti grade 1).Maelezo ya mshono wa sketi ya RINDA BOX yenye urefu wa sentimeta 30 kutoka kwenye magoti kwenda chini.



Na Suruali 2 za rangi ya damu ya mzee (kitambaa cha suti grade 1)kwa Wavulana . Maelezo ya mshono suruali yenye marinda 2,turn up na chini upana sentimeta kuanzia 16.

ii. Mashati meupe jozi mbili za mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni truck suit nyekundu 1,bukta ya kijani na t- shirt yake.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu.(kwa wasichana) na rangi nyeusi kwa wavulana.
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta ya damu ya mzee.
ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni rangi ya kijivu (kitambaa cha suti grage 1.mshono wa solo na mikono mifupi (kwa waislam mikono mirefu)iwe ndefu hadi kwenye kisigino.na kwa waislamu wawe na shungi ya rangi ya kijivu.
x. Tai ya kitambaa cha sketi/suruali na iwe ndefu.
xi. Tisheti (T-shirt) ya kijivu yenye kola ya damu ya mzee.
xii. Koti jeupe la Maabara(labaratory coat)

NB.KWA MWANAFUNZI MWENYE BIMA YA AFYA ANASHAURIWA KUJA NAYO SHULENI KWA AJILI YA KUMSAIDIA KUPATA MATIBABU PINDI AWAPO SHULENI.KWA WALE WASIO NA BIMA YA AFYA *(MZAZI ANAWEZA KUMLIPIA AU KUMPATIA MWANAE FEDHA TSH 50,400/= KWA AJILI YA KUMTENGENEZEA BIMA YA AFYA YA TOTAL AFYA CARD/ NHIF (ALIPE AKIWA SHULENI)*

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 14 caunter book (4 quire)
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na upana wa futi $2^{1/2}$
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki, blanket 1, na mto na foronya yake ya pink. 1, chandarua 1.*;*
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, hard broom 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Shule za Kutwa**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**Fedha za michango zilipwe kwenye akaunti ya shule Na.31102515078 (MKOLANI SEKONDARI SCHOOL SELF RELIANCE)Katika Benki ya NMB. Leta pay in slip halisi shuleni.**

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule EDITH R. MWEYA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0784 932097**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0719 223241**
- **Mwalimu Taaluma 0755 821128**
- **Mwandamizi Malezi 0786 897462**

**PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERMENTS**

## MKOLANI SECONDARY SCHOOL

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

Name of student...............................................................................................

To Medical Officer,

District/ Regional/ Designated Hospital.

Please examine the above named in full as to his/her physical and mental fitness for being able to pursue Advanced Secondary School Education for two years.

1. Eye Sight ........................................................................................................................
2. Hearing ..........................................................................................................................
3. Speech ...........................................................................................................................
4. Heart examination .......................................................................................................
5. Blood pressure .............................................................................................................
6. STDs..............................................................................................................................
7. Epilepsy.........................................................................................................................
8. Asthma...........................................................................................................................
9. TB ..................................................................................................................................
10. Diabetes........................................................................................................................
11. Sickle Cell....................................................................................................................
12. Tropical ulcer...............................................................................................................
13. Tumors (breast)............................................................................................................
14. Pregnancy test (for girls)..............................................................................................
15. Neurosis.........................................................................................
16. Other observation..........................................................................................................

I have examined the above named and consider him/her physically and mentally fit/unfit to pursue Secondary School Education.

NAME.......................................................................................................................
SIGNATURE ........................................................DATE .......................................................
STATION...................................................................................................................
OFFICIAL STAMP.............................................................................................................

**FOMU YA KURIPOTI SHULENI**

**SHULE YA SEKONDARI MKOLANI**

1. Tarehe ya kuingia shuleni.............................................admiddion No......................
2. Jina la mwanafunzi..............................................................................................
3. Darasa na mchepuo anaoingia...............................................................................
4. Kabila......................................................................................................
5. Tarehe ya kuzaliwa.............................................wilaya...........................
6. Jina la baba/mlezi..............................................................................................
7. Kazi ya baba/mlezi..............................................................................................
8. Namba ya simu ya baba/mlezi..............................................................................
9. Mahali baba/mlezi anapoishi.................................................................................

HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Dini/madhehebu.......................................................................................
2. Michezo aipendayo au ..............................................................................
3. Jina la baba.............................................................................................................
4. Jina la mama............................................................................................
5. Kama wazazi wamefariki ( yatima) taja jina la mtu anayeishi naye......................................
...............................................................................................................
6. Uhusiano wako na mtu anayeishi naye......................................................
   Kijiji.........................................................wilaya.......................
   Anuani yake ...........................................................................................
   Namba yake ya simu...............................................................................
7. Taja jina na uhusiano wa anayekulipia karo.................................................................
8. Tatizo la kiafya (lipo/halipo) kama lipo eleza: ...............................................................
   ...........................................................................................................................
   ..................................................................................
9. Taja ndugu wanne watakaomtembelea mwanafunzi shuleni:
   (a) Jina ................................uhusiano...........................simu.......................
   (b) Jina ................................uhusiano...........................simu.......................
   (c) Jina ................................uhusiano...........................simu.......................
   (d) Jina ................................uhusiano...........................simu.......................

Jina la mwanafunzi.......................................................sahihi yake..................

Darasa na tahasusi anayosoma............................................................................

**VITABU VYA TAHASUSI VINAVYOPENDEKEZWA**

**GEOGRAPHY**

- General geography in diagrams ( R. E Bunnett)
- Practical Geography for Africa (John M. pritchaard)
- Physical Geography for Africa ( D. T. Msabila )
- Human and Economic Geography ( D. T. Msabila)

**PHYSICS**

- S. Chand's principle of Physics – Class XI & XII-
- Principle of Physics – Rogers Municaster
- Advanced level Physics –Nelkon & parker
- Principle of physics – Tom Duncan

**BIOLOGY**

- Advanced Biology for Secondary schools – (Michael R.), Biological science – (Taylor O J& Stoud G.W)
- Cell structure and organization – L. Msaki
- Understanding Biology – Fourth edition

**ADVANCED MATHEMATICS**

- Advanced level mathematics – C. J TRANTER
- Pure Mathematics 1 & 2 – Backhouse
- Mathematics for A level ( volume 1 & 2) – S. Chand
- Advanced level Mathematics ( Vol 1) - L. K. Shayo

**CHEMISTRY**

- Advanced level physical chemistry with General Chemistry – APE network 2012, 1 St Edition 2011
- Essential of Physical Chemistry – Arun Bahl
- Organic Chemistry – Arun Bahl, 1St Edition illustrative Reversed 2012

**GENERAL STUDIES**

- General Studies for Advanced Level Certificate, Form five – Richard R.F Mbalase
- General Studies for Advanced Level Certificate, Form six – Richard R.F Mbasale

General Studies, supplementary book for advanced and collages, second edition -Konrad Adenaker S